Jina: ______________________________ Tarehe: ______________

Nambari ya mwanafunzi(**KNEC ASSESSMENT NO.**) ______________________

Gredi ______________________ Jinsia: Mvulana [ ] Msichana [ ]

Jina la shule ______________ Nambari ya Shule [ ][ ][ ][ ]

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI**

**Mwalimu ajaze mjalizo baada ya kusahihisha kazi ya mwanafunzi**

**Viwango vya kutathmini**

| **ZOEZI** | **Kuzidisha matarajio 4** | **Kufikia matarajio 3** | **Kukaribia matarajio 2** | **Mbali na matarajio 1** |
|---|---|---|---|---|
| Kusoma kwa sauti 10 | Ana uwezo wa kusoma kwa kasi bila kusita. Anazingatia alama zote za uakifisho. | Ana uwezo wa kusoma bila kusita. Anazingatia baadhi ya alama za uakifisho. | Ana uwezo wa kusoma, isipokuwa anasitasita. Hazingatii alama za uakifisho. | Hana uwezo wa kusoma maneno mengi. Hazingatii alama za uakifisho. |
| Kusikiliza na kuzungumza **(alama 5)** | **5** | **4** | **2 - 3** | **0 - 1** |
| Sarufi/Ufahamu/ kuandika **(alama 35)** | **35** | **31 - 34** | **15 - 29** | **0 - 14** |

## SEHEMU A:
## KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA


1. **Mwalimu atamsalimia mwanafunzi kisha atamwambia kuwa atamuuliza maswali naye ayajibu kwa Kiswahili.**

Jina langu ni Munira. Mimi ninasoma katika shule ya msingi ya Elimu Bora. Ninasoma katika gredi ya pili. Shule yetu ina wanafunzi mia tatu na watano. Tuko na walimu thelathini na wawili. Mwalimu mkuu anaitwa Bwana Odhiambo. Yeye ni mwalimu wa Kiswahili. Mwalimu wa darasa letu anaitwa Bi. Aremo. Yeye ni mwalimu mwema na mpole.

(a) Mwandishi wa hadithi hii anaitwa nani? **(Mwanafunzi ajibu)**
(b) Yeye yuko katika gredi ya... **(Mwanafunzi ajibu)**
(c) Shule yao ina idadi ya wanafunzi wangapi? **(Mwanafunzi ajibu)**
(d) Mwalimu mkuu wa shule yao anaitwaje? **(Mwanafunzi ajibu)**
(e) Mwalimu wa darasa la Munira anaitwa...**(Mwanafunzi ajibu)**

## KUSOMA

2. **Soma kifungu hiki kwa sauti**



Tulikuwa darasani tukicheza, ghafla mwalimu akatuuliza, "ni nini mnataka kuwa mtakapokuwa wakubwa?" Rafiki zangu wakasema kwa sauti kubwa, "mimi nitakuwa daktari," mwingine akasema, "mimi nitakuwa mwalimu, mimi nikasema, "mimi nitakuwa mwandishi." Tulicheka kwa furaha, tukiamini tutafikia malengo yetu.

## SEHEMU B:
## UFAHAMU

3. **Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali yafuatayo. (alama 5)**



Fibi ni msichana wa miaka saba. Yeye ana wazazi. Mama yake anaitwa Amia. Baba yake anaitwa Simatwa. Wao wanaishi katika mtaa wa Upendo. Fibi ana dada wawili na kaka mmoja. Dada zake wanaitwa Wakesho na Rosa. Kaka yao anaitwa Juma. Wazazi wa Fibi ni walimu. Aremo huwapa watoto wake ushauri. Yeye huwaomba wawe na adabu na heshima. Anataka wawe watiifu wote. Baba yao huwashauri wawe safi kila wakati. Nguo zao na miili yao pia iwe safi. Siku ya usafi shuleni, Fibi alituzwa zawadi ya sabuni.



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

a) Fibi anaishi katika mtaa gani? ______________________________

b) Baba wa Fibi anaitwaje? ______________________________

c) Ndugu za Fibi ni ____________________ na ____________________

d) Ni nani hupenda watoto wawe safi? ________________ **(Baba, Nyanya)**

e) Fibi alituzwa nini shuleni? ______________________________

## SARUFI

**Onyesha silabi kwenye maneno**

**Mfano: bibi = bi + bi**

1. Gari = ______________________
2. Bendera = ______________________
3. Shamba = ______________________

**Andika sentensi hizi kwa wingi.**

4. Kalamu hii. ______________________
5. Dawati hili. ______________________
6. Mimi ni mwanafunzi. ______________________
7. Kitabu chako . ______________________

**Chora vyakula hivi**

| **8.** Ndizi | **9.** Sukumawiki | **10.** Chapati | **11.** Ugali |
|---|---|---|---|
| | | | |

**Tumia 'huyo' au 'hao' kujaza nafasi.**

12. ________________ wanacheza kandanda.
13. ________________ ni mkulima hodari.
14. ________________ ni wanafunzi wazuri.

**Unda maneno ukitumia sauti hizi.**

15. gh - ______________________
16. sh - ______________________



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com


**Andika majina ya picha hizi**

17.



______________________

18.




______________________

19.



______________________

20.



______________________

**(Mwavuli, Chungu, Bendera, Jembe)**

**Chagua jibu sahihi.**

21. Mti ule ni ______________________ **(kirefu, mrefu)**
22. Matunda yale ni ______________________ **(matamu, vitamu)**
23. Kiatu kile ni ______________________ **(kikubwa, mkubwa)**

**Tumia maneno yenye adabu kukamilisha sentensi.**

24. Tafadhali mwalimu, nipe ruhusa ya kwenda______________________ **(chooni, msalani)**
25. Mama yao ______________________ juzi mtoto msichana. **(alijifungua, alizaa)**

## KUANDIKA

**Andika sentensi tano kuhusu:**

**MNYAMA NIMPENDAYE**

26. ______________________
27. ______________________
28. ______________________
29. ______________________
30. ______________________



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com